# MAJI TANZANIA

TOLEO NA 024

APRILI- JUNI, 2024


## Wizara ya Maji Namba Moja Duniani kwa kazi za miradi ya Maji

Utendaji wa Wizara ya Maji na taasisi zake umeifanya kutambulika kimataifa ndani na nje ya bara la Afrika kwa kazi na utekelezaji wa miradi ya maji.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema makubwa yaliyoitambulisha Wizara ya Maji ni pamoja na Programu ya Lipa kwa Matokeo (P4R) ambapo Tanzania imekuwa mfano kati ya nchi zaidi ya 50 na kutambuliwa na Benki ya Dunia, hali ambayo inafanya Wizara ya Maji kuwa darasa kwa nchi nyingine duniani kuja Tanzania kujifunza utekelezaji wa miradi ya maji.





## RUWASA yapongezwa kwa kazi ya ujenzi wa miradi ya maji

## Aweso atembelea Grid ya Maji ya Taifa ya nchini China

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ametembelea Gridi ya Maji ya Taifa ya China (South-to-North Water Diversion Project) lengo likiwa kuongeza weledi katika maandalizi ya ujenzi wa Gridi ya Maji ya Taifa nchini Tanzania inayolenga kutumia vyanzo vikuu ya maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa na mito mikubwa kama Rufiji kusambaza maji maeneo yenye upungufu wa vyanzo vya maji vya uhakika.



# Wizara ya Maji Namba Moja Duniani kwa kazi za miradi ya Maji

Utendaji wa Wizara ya Maji na taasisi zake umeifanya kutambulika kimataifa ndani na nje ya bara la Afrika kwa kazi na utekelezaji wa miradi ya maji.
Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema makubwa yaliyoitambulisha Wizara ya Maji ni pamoja na Programu ya Lipa kwa Matokeo (P4R) ambapo Tanzania imekuwa mfano kati ya nchi zaidi ya 50 na kutambuliwa na Benki ya Dunia, hali ambayo inafanya Wizara ya Maji kuwa darasa kwa nchi nyingine duniani kuja Tanzania kujifunza utekelezaji wa miradi ya maji.
Haya yamewekwa wazi na Waziri Aweso (Mb) wakati akiwasilisha hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa katika Mkutano wa 15 (Mkutano wa Bajeti) wa Mwaka 2024/2025 Bungeni Jijini Dodoma.
Bajeti hiyo imesheheni masuala mapya ikiwamo kuanza kutumia teknolojia ya matumizi ya Dira za maji za malipo kabla (pre-paid water meters) badala ya Dira za kulipa baada ya matumizi (post-paid water meters) ili kuhakikisha uendelevu wa huduma ya maji vijijini na mijini.



Ameainisha jingine kubwa ni kupatikana kwa chanzo kipya cha fedha za utekelezaji wa miradi ya maji kupitia Hatifungani ambapo Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tanga imekuwa ya kwanza kuzindua uuzaji wa Hatifungani ya Kijani yenye thamani ya Shilingi bilioni 53.12.
Akizungumzia vipaumbele vya Wizara ya Maji, Waziri Aweso amesema ni pamoja na kuimarisha matumizi ya mitambo ya uchimbaji wa visima na mabwawa ili kufikisha huduma kwenye vijiji ambavyo havina huduma pamoja na kutekeleza Programu ya kuchimba visima 900 kwa maana ya kila jimbo la uchaguzi kupata visima vitano, na ujenzi wa mabwawa madogo madogo.

“Wizara imeweka vipaumbele ambavyo vitazingatiwa katika mpango na bajeti ya mwaka 2024/25 ili kufikia lengo la kuwapatia huduma ya majisafi na salama kwa zaidi ya asilimia 85 ya wananchi wa vijijini na zaidi ya asilimia 95 ya wakazi wa mijini,” Waziri Aweso amesema.

Sambamba na hilo, amesema Wizara ya Maji imejipanga kupunguza upotevu wa maji kwa kufanya ukarabati wa miundombinu ya maji iliyochakaa na kudhibiti wizi wa maji; kufunga dira za maji ya jumla (bulk meters); kufunga dira za maji kwa wateja wote; kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kulinda miundombinu ya maji na kuwachukulia hatua stahiki wanaojihusisha na wizi wa maji na uharibifu wa miundombinu.

“Lengo ni kupunguza kiwango cha maji yanayopotea kutoka wastani wa asilimia 35.3 hadi kufikia kiwango kinachokubalika kimataifa cha asilimia 20,” Waziri Aweso ameweka bayana.

# Mradi wa Maji wa Same – Mwanga wafikia asilimia 90, Waziri Aweso awasha pampu kusukuma maji

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amewasha pampu ili kusukuma maji kwenda katika tanki la Kivengere ambapo ujenzi wa mradi huo umefika asilimia 90 ya utekelezaji.
Waziri Aweso amekagua mradi huo mwanzo hadi mwisho na kuona utekelezaji wake kwa kushudia kukamilika kwa mifumo ya kutibu maji na kisha akafanya zoezi la kuwasha pumpu za kusukuma maji kupeleka kwenye tanki la maji la Kiverenge.

Katika ukaguzi huo, amefika eneo la Lembeni na kuona shughuli ya kupitisha bomba kuvuka chini ya barabara kubwa inayoelekea Moshi na kuelekeza kazi hiyo ikamilike ndani ya masaa 24 ili wananchi wapate huduma ya maji.

Ukaguzi uliofanywa na Waziri Aweso ni utekelezaji wa maagizo ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia kwa Makamu wa Rais Mhe Dkt. Philip Mpango katika kuhakikisha mwisho wa mwezi Juni 2024 wananchi wa Same - Mwanga wanapata huduma ya uhakika ya majisafi na salama.
Waziri Aweso ameshuhudia mazingira magumu ya kazi katika kumaliza ujenzi wa mradi na ameridhishwa na morali pamoja na kasi iliyipo katika kufanikisha kazi hiyo na amewahakikishia wananchi wa Same-Mwanga-Korogwe kazi hiyo itakamilika kwa wakati kama maelekezo yalivyotolewa kuhusu kukamilisha mradi huo.





# Aweso atembelea Grid ya Maji ya Taifa ya nchini China

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ametembelea Gridi ya Maji ya Taifa ya China (South-to-North Water Diversion Project) lengo likiwa kuongeza weledi katika maandalizi ya ujenzi wa Gridi ya Maji ya Taifa nchini Tanzania inayolenga kutumia vyanzo vikuu ya maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa na mito mikubwa kama Rufiji kusambaza maji maeneo yenye upungufu wa vyanzo vya maji vya uhakika.

Ametembelea eneo hilo ikiwa ni sehemu ya kushiriki Kongamano la Kumi na Tano la Ujenzi na Uwekezaji katika Miundombinu.
Gridi ya Maji ya Taifa ya China ina njia kuu tatu ambazo ni Mashariki, Kati na Magharibi zenye jumla ya urefu wa kilometa 4,350. Wakati sehemu ya Magharibi ya Gridi hiyo ipo katika hatua za awali katika mipango, njia ya Mashariki (kilometa 1,466) na njia ya Kati (kilometa 1,432) zikiwa zimekamilika. Njia hizo kwa pamoja zinahudumia zaidi ya wanufaika milioni 140 katika miji mikubwa na midogo zaidi ya 40 pamoja na majimbo na wilaya zaidi ya 280 katika maeneo mbalimbali ikiwamo jiji la Beijing na Tianjin.

Ziara hiyo iliyohusisha wataalam wengine wa Sekta ya Maji ni fursa kwa Tanzania katika kuboresha ujenzi wa Gridi ya Maji ya Taifa kwa matumizi ya sasa na vizazi vijavyo.









# Hati fungani ya kwanza kusini mwa jangwa la Sahara yaingia soko la Hisa la Dar



Hati Fungani ya Kijani ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA) hatimaye imeingia sokoni rasmi katika soko la hisa la Dar es salaam, na kuwa Taasisi ya kwanza ya umma inayotoa huduma katika jamii kuingia katika soko hilo.

Tanga UWASA inakuwa Mamlaka ya maji ya kwanza katika taasisi za Umma kuingia katika soko la la Hisa kwa nchi za Kusini mwa jangwa la Sahara, hivyo kuifanya Tanzania kuwa nchi ya mfano na darasa kwa nchi nyingine..
Waziri wa Ujenzi Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) ambaye pia ni mtaalamu wa masoko ya hisa ameongoza kazi hiyo kwa niaba ya Waziri wa Fedha Mhe. Mwigulu Nchemba(Mb) jijini Dodoma.

Mhe. Bashungwa ameishukuru Wizara ya Maji na serikali kwa ujumla kwa kuingia katika utaratibu huo na kuzitaka taasisi nyingine za serikali kuiga mfano huo na kusema itasaidia serikali kusonga mbele kwa kupata chanzo mmbadala cha fedha badala ya kutegemea bajeti ya serikali.
Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ambaye amehudhuria hafla hiyo amewapongeza Tanga UWASA kwa kutafsiri maono ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan la kuhakikisha akina mama wote nchini wanapunguziwa majukumu kwa kufikishiwa huduma ya maji katika maeneo yao "kumtua mama ndoo yam aji kichwani".

Akizungumza katika hafla hiyo Mkurugenzi Mtendaji Tanga UWSSA Mhandisi Geofrey Hill amesema malengo ya awali ilikuwa kukusanya shilinigi Bilioni 53.1 ambapo kiasi kilichokusanywa kilifika shilingi Bilioni 54.72.
Amesema fedha hizo zitasaidia kupanua miundombinu ya maji ikiwemo ujenzi wa tenki kubwa lenye uwezo wa kuhifadhi lita za ujazo milioni 35 . Aidha, upanuzi huo utawezesha maji kupatikana kwa asilimia 100 Tanga mjini wakati huduma ya maji katika miji mingine inayohudumiwa na Tanga UWASSA itafikia asilimia 95 badala ya asilimia 70 zinazotolewa sasa.

Eneo jingine litakaloboreshwa kwa wananchi ni utoaji wa huduma ya Dira za maji za malipo kabla ambapo Dira 10,000 zitanunuliwa. Pia, uzalishaji maji utaongezeka kutoka lita za ujazo elfu 45 hadi lita elfu 60 na kupunguza upotevu wa maji kutoka asilimia 30 hadi 20.. Uzinduzi wa Hati fungani ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga ulifanyika jijini Tanga Februali 22, 2024 ukiongozwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdori Mpango.

# Tanga UWASA yapewa pongezi kwa matokeo ya mauzo ya Hatifungani







Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ametoa pongezi kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanza (Tanga UWASA) kwa matokeo mazuri ya mauzo ya Hatifungani ya kijani ya miundombinu yam aji.

"Nawapongeza kwa dhati Mamlaka yetu ya Maji Tanga kwa kufanikisha mauzo ya asilimia 103 ya Hatifungani ya Kijani ya miundombinu ya maji Tanga ambapo zaidi ya shilingi za Tanzania bilioni 54.72 zimekusanywa kutoka kwa wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi ikiwa matarajio yetu yalikuwa bilioni 53.12 na kwa hili tumevuka lengo na haya ni mafanikio makubwa sana.

Hili ni wazo la Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan na mnamo terehe 22 Februari, 2024 aliwakilishwa na Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango katika uzinduzi wake.

Kwa sasa tupo hatua ya matokea na mauzo na hatua nyingine zitafuata.

Haya ni mapinduzi makubwa sana katika sekta yetu ya maji yenye lengo la kufanikisha upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi, kwa hakika sekta ya maji imeandika historia mpya Tanzania na Afrika Mashariki na Kati kwa ubunifu huu.

Mwanzo jambo hili lilionekana haliwezekani lakini niliwasisitiza tuthubutu na tutaweza na hakika tumeweza.

Fedha hizi zilizopatikana zinaenda kuwezesha utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wakazi wa jijini Tanga pamoja na miji ya Muheza, Pangani na Mkinga sambamba na kuimarisha usimamizi na utunzaji wa vyanzo vya maji.

Shukran za dhati ziende kwa Rais wetu Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kutuongoza vyema na hata kununua Hatifungani hii.

Pia, asanteni wadau wote walioshiriki katika ununuzi wa Hatifungani ya TangaUWASA na hongera kwa Mbunge wa Jimbo la Tanga na Waziri wa Afya Mhe Ummy Mwalimu (Mb) kwa kuwa sehemu ya hamasa na kufanikisha jambo hili."

Kutoka kwa Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb)

# Mifumo ya TEHAMA ya Maji kusomana

Wataalamu wa mifumo ya TEHAMA wa Wizara ya Maji wamepongezwa kwa kuanza kazi ya kuitengeneza mifumo yote katika wizara kusomana.

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Kundo Mathew (Mb) ametoa pongezi hiyo baada ya kutembelea timu inayofanya kazi hiyo na kuongea nayo.

"Kazi hii itaondoa utitiri wa mifumo na kuondoa changamoto ya utekelezji wa majukumu" Mhandisi Kundo amesema.

Amesema kazi hiyo ya kuunganisha mifumo ili isomane iharakishwe ikienda sambamba na ujenzi wa mfumo wa pamoja wa Dira za malipo ya kabla ya matumizi ( Universal Vending systems for Prepaid Water meter).

Amesema kiu kubwa ya viongozi ni kuona sekta inaondoka katika matumizi ya Dira za kawaida (mechanical meters )na kuingia katika matumizi ya Dira za malipo ya kabla (Smart Prepaid Meter) kama alivyoelekeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Lengo la mfumo ni  pamoja na kuwezesha Dira za maji za kisasa (smart prepaid water meters) kufanya kazi kwa tja ili kuondokana na malalamiko ya wateja kudai kubambikiwa bili na kuepusha kiwango cha upotevu wa maji .





# RUWASA yapongezwa kwa kazi ya ujenzi wa miradi ya maji

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Kundo Mathew (Mb) ameipongeza Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa mchango mkubwa kwenye mapinduzi ya huduma ya maji vijijini.

Mhe.Kundo ametembelea makao makuu ya RUWASA jijijini Dodoma pamoja na mambo mengine amewataka watendaji wa RUWASA kutochoka kufanyakazi.
"Bila kupepesa macho, Sisi tuliokuwa nje ya sekta ya maji tunajua hali ya huduma ya maji vijijini ilivyokuwa kabla ya kuanzishwa kwa RUWASA na hali ilivyo hivi sasa, Hongereni sana."

Akiongelea suala la kuwajibika, Mhe. Kundo amesema kuwa "sisi sote ni wasaidizi wa Mheshimiwa Waziri sio mimi peke yangu, kila mmoja akiongeza bidii kwenye eneo lake tutamimiza ndoto za Waziri na hivyo kutimia ndoto za Rais wetu".

Pia Naibu Waziri Kundo ameitaka RUWASA kuongeza bidii na kukamilisha miradi ambayo imebakiza vitu vidogo vidogo ili ikamilike na kuleta matokeo makubwa.

Kwa upande wa dira za maji, ameitaka RUWASA kuwa na mkakati madhubuti wa matumizi ya dira za maji za malipo kabla ya matumizi (pre paid meters) kama ilivyoagizwa. Amesema ni muhimu kwa RUWASA kuwa na mkakati utakaohakikisha kila mteja mpya anafungiwa dira ya maji ya malipo kabla ya matumizi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA Mhandisi Clement Kivegalo amemshukuru Naibu Waziri Kundo kwa kutenga muda pamoja na majukumu mazito ya vikao vya bunge vinavyoendelea kuja kuongea na RUWASA.

Tangu kuanzishwa kwa RUWASA tarehe 1 Julai , 2019 jumla ya wananchi 17,416,1111 wa vijijini wamefikiwa na huduma ya maji kwenye maeneo yao.





# Mkataba wa kutoa maji ya ziwa Victoria Kahama hadi Ushetu wasainiwa rasmi, thamani yake zaidi ya Bilioni 44

Hafla ya utiaji saini imeshuhudiwa na Waziri wa Fedha Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb) na Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), Ushetu.

Mradi huo mkubwa wa maji unathamani ya zaidi ya shilingi bilioni 44 na utaanza utekelezaji hivi karibuni na unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 24.

Utekelezaji utahusisha ujenzi wa matanki matatu (3) yenye ujazo wa lita 500,000; 300,000 na 100,000 katika maeneo tofauti ndani ya Kata ya Ulowa.

Pamoja na ujenzi wa bomba kuu lenye kipenyo cha kuanzia milimita 350 hadi milimita 100 lenye urefu wa kilometa 76 kutoka Manispaa ya Kahama kwenda Ulowa hadi kwenye matanki.
Pia ujenzi wa mfumo wa kutibu maji na ujenzi wa vituo 35 vya kuchotea maji na ujenzi wa mfumo wa usambazaji maji wenye bomba aina HDPE zenye urefu wa KM 74 pamoja na vituo vya kuchotea maji 35.

Pamoja na uunganishaji wa wateja wa majumbani 1,000 wa awali kwa wateja wa majumbani. Ili kufanya mradi kuwa endelevu, mradi huo utahusisha ujenzi wa jengo la ofisi kwa ajili ya Chombo kitakachoundwa kuendesha mradi na kuwahudumia wananchi baada ya mradi kukamilika na vifaa vya moto (pikipiki)
Mradi utatekelezwa na Mkandarasi Kampuni ya SIHOTECH ENGINEERING COMPANY LTD ya Jijini Dar Es Salaam kwa kushirikiana na Kampuni ya MPONELA CONSTRUCTION COMPANY LTD ya Iringa kwa gharama za Mkataba jumla ya Shilingi 44,271,886,678.17.

Manufaa ya mradi ni pamoja na kuboresha afya ya wananchi, utachochea kwa kiasi kikubwa maendeleo ya Halmashauri ya Ushetu kwani utatoa fursa kwa wananchi kujihusisha na shughuli zingine za kiuchumi badala ya kutumia muda mrefu kutafuta maji, kama inavyofanyika sasa. Mradi huu pia utakuwa kichocheo cha maendeleo ya wananchi.

Mradi umesanifiwa kuhudumia wananchi wapatao 189,836 wa Kata za Igunda, Kisuke, Kinamapula, Nyamilangano, Mapamba, Uyogo, Bukomela, Ushetu na Ulowa.





# Wakurugenzi wa mamlaka ndogo za maji wapewa shule





Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri akikagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa maji wa Same Mwanga Korogwe.

Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri amefungua kikaokazi cha mafunzo kwa Wakurugenzi watendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za wilaya na miji midogo,.

Mafunzo hayo yanafanyika katika ukumbi wa wizara Mtumba

Katika hotuba yake Mhandisi Waziri ameeleza kufurahishwa na mafunzo hayo yanayolenga kuwajengea uwezo katika usimamizi bora wa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira yatakayo wasaidia katika kutatua changamoto zakiutendaji katika maeneo yao ya kazi

Mhandisi Waziri amesisitiza masuala yatakayo wasaidia watendaji wa mamlaka hizo kuweza kufikia malengo yao ni pamoja na upenda na ushirikiano kwa kuzingatia maadili ya kazi na kuimarisha ushirikiano na mamlaka nyingine za serikali

Ili kutimiza azma ya kuwapatia wananchi huduma bora ya majisafi na salama kwa asilimia 95 mijini na 85 vijijini ifikapo 2025





# Katibu Mkuu Maji awataka Wahandisi washauri Mradi wa maji wa ziwa Victoria-Dodoma kutumia weledi

Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri amewataka Wahandisi Washauri wa mradi wa kutoa maji ziwa Victoria kwenda katika Jiji la Dodoma kuhakikisha wanazingatria weledi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Agizo hilo amelitoa leo katika kikao cha maandalizi ya Upembuzi Yakinifu, Usanifu wa Kina wa mradi na Uandaaji wa Makbrasha ya zabuni kilichofanyika jijini Dodoma katika ofisi za wizara zilizoko mji wa serikali Mtumba.

Amesema wananchi wa Dodoma wamesubiri kwa muda mrefu utekelezaji wa mradi huo, sasa ni muda muafaka wa kuanza kuona matunda ya serikali ambayo kwa muda wote imejipambanua kama serikali ya wananchi.

Amesema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ameelekeza wizara kuhakikisha mradi huo unaanza ili kuondoa kabisa changamoto ya huduma ya maji katika Jijila Dodoma ambalo ni makao makuu ya Nchi.

Aidha, amesisitiza ushirikishwaji wa kutosha wa wataalamu wa wizara ili kuongeza maarifa na uelewa wa kutosha wa miradi mikubwa ya maji.

Wataalamu washauri waliopewa jukumu la mradi wa ziwa Victoria kweda Dodoma ni Dong Myeong Engineering Consultants kutoka Korea Kusini pamoja na kampuni za Tanzania ambazo ni Don Consult LTD na Supelit Consulting LTD.





# MWAUWASA yapewa heko kwa kazi nzuri

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) imepongezwa kwa utekelezaji mahiri wa miradi ya maji inayolenga kuimarisha upatikanaji wa huduma ya majisafi na uimarishaji wa usafi wa mazingira kwa wananchi.

Pongezi zimetolewa na Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Nyamagana wakati wa ziara ya Kamati hiyo kujionea utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya maji maarufu kama mradi wa matokeo ya haraka (quick win) katika Kata ya Luchelele pamoja na Mtambo wa uchakataji Majitaka (DEWATS) katika Gereza la Butimba.

Kamati hiyo ilijumuisha viongozi mbalimbali wa Serikali akiwemo Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana Mhe. Amina Makilagi, na imesema MWAUWASA imefanya kazi nzuri na inayoridhisha katika utekelezaji wa miradi hiyo itakayoleta manufaa kwa wakazi wa maeneo husika.

"Kwanza tumpongeze Kaimu Mkurugenzi wa MWAUWASA, kwa kweli tangu amefika tunaona jitihada za kila siku za kuhakikisha huduma yam aji inaimarika, mara kadhaa mimi mwenyewe tumekua tukiwasiliana na umekua ukiwafikia wananchi na kupokea changamoto kwa ajili ya kuzipatia ufumbuzi, tunakupongeza kwa hili," Mhe. Peter Begga Mwenyekiti wa Kamati ya Siasa Wilaya ya Nyamagana amesema.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana Mhe Amina Makilagi amesema pamoja na pongezi hizo Serikali kupitia Watumishi wake itaendelea kufanya kazi kwa bidii ili kutoa huduma bora kwa wananchi.





Kaimu Mkurugenzi wa MWAUWASA Bi. Neli Msuya akizungumza na ujumbe huo amesema MWAUWASA inaendelea na jitihada za kuhakikisha huduma yam aji inafika katika maeneo yote ambayo yalikuwa hayajafikiwa kikamilifu.

# Ngara; Wadau wajengewa uwezo utunzaji wa Rasilimali za Maji



Wadau wa usimamizi wa rasilimali za maji wamekutana wilayani Ngara mahsusi kuhusu kuongeza ujuzi katika utunzaji wa vyanzo vya maji.

Meneja wa Idara ya Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Jumuiya za Watumia Maji, Bonde la ziwa Victoria Mhandisi Jane Mrosso amesema lengo ni kujadili na kuzipatia ufumbuzi wa pamoja changamoto zinazoathiri utunzaji wa vyanzo vya maji hususani katika mto Ruvuvu na Akagera.

Amesema jumuiko hilo ni fursa ya kipekee kwa washiriki kujifunza na kuongeza ujuzi na uelewa wa masuala mbalimbali yanayohusu utunzaji wa rasilimali za maji.

Mrosso ameongeza kuwa ujio wa wataalam wa Bodiya Ziwa Victoria wilayani Ngara ni azma ya utunzaji wa vyanzo vikuu vya maji ambavyo ni Mto Akagera ambao unaungana na Mto Ruvuvu kutengeneza Mto Kagera, pia mito hiyo ni shirikishi, hivyo maji yake yanatumiwa na nchi ya Tanzania, na majirani nchi za Burundi na Rwanda.

Ameongeza kuwa, timu ya wataalamu wa Bodi ya Ziwa Victoria, pamoja na mambo mengine watafanya zoezi la kuweka mipaka katika mito hiyo miwili (Akagera na Ruvuvu), kupanda miti rafiki wa maji na kuweka mabango ya katazo ya shughuli za kibinadamu ndani ya mita 60.

Zoezi litafanyika kwa kuwashirikisha wananchi wa maeneo husika katika kata za Nyamiaga, Rusumo na Mulukurazo na vijiji vya Rusumo, Mshikamano, Bulengo, Kagali na Kyenda.

Mhandisi Mrosso amewasisitiza washiriki watumie fursa hiyo kujadili kwa kina na kutoa michango na hoja zinazojikita katika usimamizi wa rasilimali za maji.

Washiriki wa tukio hilo ni pamoja na viongozi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ngara, viongozi wa kisiasa kutoka mamlaka za Serikali za Mitaa, Kamati ya usalama, Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri, Mamlaka za maji na RUWASA, TFS, TANESCO, Maafisa Tarafa, Vyombo vya Watumia Maji (CBWSO) na AZAKI.

# Mbio ya Kuleta Mabadiliko ya Huduma ya Maji: Wazalishaji wa Dira za Malipo Kabla watembelewa na AWESO





Waziri wa Maji Mhe Jumaa Aweso (Mb) ametembelea viwanda mbalimbali vya kutengeneza na kuzalisha Dira za Maji za Malipo Kabla nchini China ili kujionea teknolojia inayotumika katika kutengeneza wake.

Waziri Aweso akiongelea mkakati wa Wizara ya Maji amesema wataalamu alioongozana nao wataungana na Kamati maalum iliyoundwa Wizarani na kwa pamoja kuwa na muongozo wa namna ya utekelezaji wa mabadiliko kufanyika hatua kwa hatua baada ya kujionea uzalishaji na aina mbalimbali za Dira

Amesema ni wakati sahihi wa kutekeleza agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kuhusu mabadiliko ya Dita za Maji kutoka zile za kawaida na kuanza kutumia za kisasa za Malipo kabla.

Mhe. Aweso amesema pamoja na uhitaji wa mageuzi upo umuhimu wa kujiridhisha na kufanya utafiti wa kutosha kuhusu Dira sahihi kwa ajili ya matumizi ya Tanzania kwa kuzingatia ubora, uzalishaji toshelevu, uendelevu na thamani ya fedha ili zisiwe changamoto kwa wananchi.

Waziri Aweso amefanya ziara hiyo katika viwanda vya jiji la Shangha akiwa ameambatana na timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Maji ikiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara Mhandisi Mwajuma Waziri.

# Tanzania yapeperusha bendera ajenda ya maji kwa ustawi wa wote jijini Bali

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), amemuwakilisha Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Kongamano la 10 la Maji Duniani (10th World Water Forum) linalofanyika jiiini Bali nchini Indonesia.

Katika Mkutano wa Ngazi ya Juu , ulioongozwa na Rais wa Indonesia Mhe. Joko Widodo,  pamoja na Wakuu wa Nchi na Serikali kutoka mataifa mbalimbali Duniani, Tanzania imeithibitishia Dunia kuhusu utashi na uongozi wake katika kutatua changamoto za maji.

Baada ya Waziri wa Maji kuwasilisha kauli na tamko la Tanzania kwa niaba ya Mhe Rais Samia lililoelezea utekelezaji na mikakati inayoakisi kaulimbiu ya kongamano ya Maji kwa ustawi wa pamoja, Mataifa mbalimbali yameipongeza Tanzania kwa kazi kubwa inayoendelea kufanyika na mikakati iliyojiwekea kufikisha huduma ya maji kwa wananchi.

Akiwasilisha tamko la nchi ya Tanzania Mhe. Aweso amesema Kaulimbiu ya Kongamano hilo “maji kwa ustawi wa pamoja (water for shared prosperity),” inaonesha umuhimu wa maji katika utu, maisha na maendeleo katika nyanja za afya, elimu, ajira, amani, utulivu wa kijamii na hifadhi ya mazingira.

Waziri Aweso amebainisha umuhimu wa mdahalo wa kitaifa na kimataifa kuhusu maji na kuiweka agenda ya maji katika vipaumbele vya kitaifa na mikutano ya kimataifa kama vile Umoja wa Mataifa na World Economic Forum. “Wakati wa maamuzi ni leo, wakati wa uongozi wa kisiasa kutatua matatizo ya maji ni leo”  Mhe. Aweso amesema.






Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ameshiriki katika mdahalo nchini China  kuhusu teknolojia za ujenzi wa miundombinu ya miradi ya  maji  inayohimili mabadiliko ya tabianchi.

Mdahalo umefanyika katka Kongamano la Kumi na Tano la Uwekezaji katika Ujenzi wa Miundombinu, ambapo pia imehusu kupunguza uzalishaji wa he

Mhe. Aweso amebainisha kuwa kwa sasa sehemu kubwa ya kazi ya usambazaji maji nchini Tanzania zinahusisha ujenzi wa miradi yakiwemo matanki na mabwawa.

Ameikaribisha Jumuiya ya Kimataifa, ikiwanmo nchi ya China kushirikiana na Wizara ya Maji katika ujenzi wa Gridi ya Maji ya Taifa, Ujenzi wa kiwanda cha mita za maji za malipo kabla na uboreshaji wa teknolojia za kudhibiti mivujo ya maji.

Wizara ya Maji Tanzania ni miongoni mwa Sekta zilizoalikwa kushiriki katika Kongamano hilo linalohusu uwekezaji katika ujenzi wa miundombinu inayozingatia usimamizi wa mabadiliko ya tabianchi



# Bilioni 18 kupeleka huduma ya Maji Kibamba



Serikali yatoa suluhu ya muda mfupi na muda mrefu kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 18 wa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa majisafi kwenye katika kata ya Mbezi ambayo itaenda kuhudumia wakazi takribani 144,000

Huu ni mojawapo ya utekelezaji wa mkakati wa Serikali ya awamu ya Sita ya kuboresha upatikanaji wa huduma ya Majisafi kwa mijini kwa asilimia 95 ifikapo mwaka 2025 kama inavyoeleza katika ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Akizungumza wakati wa mkutano wa hadhara na Wananchi wa eneo la Mbezi Msumi Mkoani Dar es salaam, Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Andrew Kundo (Mb) amesema kuwa uwekezaji huu ni mojawapo ya mkakati wa Serikali wa kuhakikisha eneo lote la Kibamba linapata majisafi na kwa uhakika.

Ameongeza Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhamiria kuhakikisha anawatua ndoo kichwani Wananchi wa Jimbo la Kibamba ikiwemo eneo la Msumi kwa kutenga jumla ya Bilioni 18 ambazo zitatumika kuboresha huduma ya majisafi.

Mhandisi Kundo amesema kuwa kata ya Mbezi ni moja ya eneo korofi ambalo wananchi wamekuwa kwenye changamoto ya maji kwa muda mrefu, hivyo ni wakati sahihi kupata huduma bora na ya uhakika ambapo ameelekeza uchimbwaji wa visima katika eneo la Msumi kama mpango wa muda mfupi wakati utekelezaji wa mradi huo wa Bilioni 13 ukiwa unaendelea.

Kwa upande wake, Mbunge wa Kibamba, Mhe. Issa Mtemvu amesema uhitaji wa Wananchi wa Jimbo la Kibamba ni huduma ya Maji iliyo bora hivyo ni faraja kusikia mipango ya kuboresha upatikanaji wa majisafi katika eneo hilo.

“Tunakushukuru Naibu Waziri kwa kufika katika eneo la Msumi ambalo ni kati ya maeneo yanayopatikana katika Jimbo la uchaguzi wa Kibamba, Tunaamini ujio wenu unakwenda kutupa suluhisho la hutaki letu la muda mrefu.”ameeleza

Nae Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Ndugu Kiula Kingu amesema kuwa DAWASA imepanga kutekeleza mradi huo utakaohusisha ujenzi wa tenki la Lita milioni 6 pamoja na kituo cha kusukuma maji eneo la Kibamba ambao pia utanufaisha eneo la Mbezi Msumi.

Ameongeza kuwa utekelezaji wa kazi hiyo utagharimu jumla ya Bilioni 13 huku pia kukiwa na fedha ya Tsh Bilioni 5 iliyotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kuboresha huduma ya Maji katika mkoa wa Dar es Salaaam.

“Tunatambua changamoto iliyopo katika eneo hili, kama Mamlaka tayari tumeshafanya usanifu wa mradi ambao tunaamini unakwenda kutatua changamoto ya eneo hili”ameeleza.

# Waziri Aweso awahakikishia ushirikiano Watumishi wa Sekta ya Maji,

- Kupendana na Kuheshimu Weledi muhimu

Waziri Wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amezindua Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Maji na kuwataka wahakikishe wanafanya kazi kwa upendo na ushirikiano ili kuleta mafanikio.




Amesema Sekta ya Maji imepiga hatua kubwa kutokana na ushirikiano ambao umejengwa na kukuzwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Saluhu Hassan, ambaye amekuwa mstari wa mbele katikq kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji "kumtua mama ndoo ya maji" .

Amesema viongozi wa Sekta ya Maji wanatambua jitihada kubwa zinazofanywa na watumishi wa wizara katika kuhakikisha huduma ya majisafi na salama inafikishwa kwa Watanzania na kwamba wataendela kuongoza kwa kuhakikisha mazingira ya kazi yanaendelea kuboreshwa kwa watumishi ili kupata matokeo.

Amesema yapo mafanikio mengi ambayo wizara inapaswa kujivunia na kwamba hayo yote yametokana na ushirikiano mkubwa ambao wanapaswa kuuendeleza baina yao katika ngazi zote




Baraza la Wafanyakazi limehudhuriwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri, (ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza) na Naibu Katibu Mkuu Bi. Agnes Meena ambao wote kwa pamoja wamewahakikishia wafanyakazi wataendela kuhakikisha kila mtumishi anapata haki yake na kuwekewa mazingira mazuri ya kutekeleza majukumu ya kazi kwa ubora unaotakiwa.

# Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akiwa jijini Dar es salaam kukagua hali ya upatikanaji wa huduma yam aji kwa wateja.







# Tuangalie fursa na kuondosha changamoto

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Bi. Agness Meena amewataka wadau wa Bonde la ziwa Victoria kuangalia fursa ili kunufaisha jamii, pamoja na kuondosha changamoto zilizopo.

Amesema hayo jijini Dar es salaam akifungua mkutano wa ngazi ya juu wa kisekta kuhusu uwekezaji wa muda mrefu, mafanikio na changamoto katika bonde la ziwa Victoria. "Jukumu kubwa sio kukabiliakana na changamoto peke yake, ila kutumia fursa zilizopo ili kuinufaisha jamii inayohudumiwa" Meena amesema.

Pamoja na wengine , kikao hicho kilichoandaliwa na Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria kimewakutanisha wajumbe kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki , Kamisheni ya Bonde la ziwa Victoria, Chama cha Wavuvi wa Ziwa Victoria, Benki ya Dunia na wadau wa maendeleo






Muwakilishi wa Benki ya Dunia, Makao Makuu ya New York nchini Marekani Bi. Toyoko Kodama akifungua bomba la maji katika kituo cha kuchotea maji cha umma katika mradi wa maji wa Labay unaohudumia vijiji viwili vya Labay na Qatabela vyenye jumla ya wakazi zaidi ya elfu tatu, Mbulu, mkoani Manyara.

Jarida Tando



**Kitengo cha Mawasiliano**

Tovuti: www.maji.go.tz